TANGAZO LA SERIKALI Na. 34 la tarehe. 17/1/2025

SHERIA YA NGUVU YA ATOMU,
(SURA YA 188)

# KANUNI

*(Zimetengezwa chini ya kifungu cha 70)*

MAREKEBISHO YA KANUNI ZA KINGA YA MIONZI IONISHI NA ISIYO IONISHI ZA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 840 la 2023

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Kinga ya Mionzi Ionishi na Isiyo Ionishi za Mwaka 2025 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Kinga ya Mionzi Ionishi na Isiyo Ionishi za Mwaka 2023 ambazo katika Kanuni hizi zinarejewa kama "Kanuni kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 3

**2**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 3, kwa-

(a) kuongeza maneno “cha Sheria” mara baada ya tarakimu “5” iliyopo mwishoni mwa tafsiri ya neno “Tume”; na
(b) kuongeza kulingana na mpangilio wa kialphabeti tafsiri ya msamiati mpya kama ifuatavyo:

> ““idhini” maana yake ni ruhusa inayotolewa katika hati na Tume kwa mtu aliyewasilisha ombi la kufanya kazi au kitendo kingine chochote kilichobainishwa katika wajibu wa jumla wa utendaji chini ya Sheria na inaweza kuwa katika namna ya usajili au leseni;”.

Marekebisho ya kanuni ya **7**

**3**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 7(3)(d) kwa kufuta maneno “katika uwanda wa spektramu ya milimita 1 hadi kilomita 1000 zitasamehewa katika

Kanuni hizi kama ilivyoainishwa" yaliyopo katika aya (d) na badala yake kuweka maneno "vitasamehewa kwenye Kanuni hizi, iwapo vitakidhi masharti yaliyobainishwa".

Marekebisho ya kanuni ya 8

**4.** Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 8 kwa kufuta kanuni ndogo ya (1) na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"(1) Mtu anayekusudia kutumia, kuingiza nchini, kusafirisha nje ya nchi, kusafirisha na kuondoa chanzo cha mionzi au nyuklia atatoa taarifa ya maandishi kwa Tume ikianinisha yafuatayo:

(a) aina ya chanzo;
(b) maelezo ya sehemu ambapo chanzokitatumika;
(c) orodha ya wataalum wenye sifa watakao endesha mtambo au kutumia chanzo; na
(d) dhumuni la kutumia chanzo.".

Marekebisho ya kanuni ya 13

**5**. Kanuni kuu inapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta kanuni ya 13 na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"Kurekebisha, kusimamishwa na kufutwa kwa idhini

**13**.-(1) Mmiliki wa leseni au aliyesajiliwa anaweza kuiomba Tume kwa maandishi kurekebisha taarifa zozote zilizopo katika leseni au cheti cha usajili.

(2) Tume inaweza, baada ya kupokea maombi chini ya kanuni ndogo ya (1)-

(a) kurekebisha kasoro iwapo itajiridhisha kuwa kuna sababu za msingi za kufanya marekebisho hayo; au

(b) kukataa kufanya marekebisho na kutoa sababu za kukataa huko.

(3) Tume inaweza kusimamisha au kufuta leseni au cheti cha usajili endapo mmiliki wa leseni au aliyesajiliwa anashindwa kuzingatia masharti kama yalivyowekwa katika Sheria na kanuni zilizotengenezwa chini yake.

(4) Endapo Tume inakusudia kusimamisha au kufuta leseni au cheti cha usajili-

(a) itamtaarifu kwa maandishi mmiliki wa leseni au aliyesajiliwa ikielezea sababu ya kusimamishwa au kufutwa kwa leseni au cheti hicho; na

(b) ndani ya siku saba kutoka tarehe ya taarifa, itampa mmiliki wa leseni au aliyesajiliwa nafasi ya kusikilizwa.

(5) Endapo Tume haijaridhika na sababu zilizotolewa na mmiliki wa leseni au aliyesajiliwa chini ya kanuni ndogo ya (4) itafuta leseni au cheti cha usajili.

(6) Mmiliki wa leseni au aliyesajiliwa ambaye leseni au cheti cha usajili kimefutwa atarejesha leseni au cheti hicho kwa Tume.”.

Marekebisho ya kanuni ya 48

**6.** Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 48, kwa-

(a) kuongeza maneno "kulingana na utoaji wa dozi iliyopangwa kwenye eneo lililolengwa ndani ya vihimili vinavyohitajika" mwishoni mwa kanuni ndogo ya (5); na

(b) kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (6) kanuni ndogo mpya kama ifuatavyo:

"(7) Mmiliki wa leseni atahakikisha upatikanaji wa kutosha wa-

(a) madaktari wenye sifa wa dawa za nyuklia;

(b) wafamasia wenye sifa wa dawa za nyuklia; na

(c) wataalamu wa teknolojia ya matibabu ya mionzi wenye sifa,

katika idara za dawa za nyuklia.

(8) Mmiliki wa leseni au aliyesajiliwa atahakikisha kwamba tathmini za ndani kwa misingi ya vipimo zinafanywa katika vipindi vilivyoidhinishwa kwa taratibu za radiolojia ambazo viwango vya marejeo ya uchunguzi vimeanzishwa.".

Marekebisho ya kanuni za 59

**7**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 59 kwa kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (2) kanuni ndogo mpya kama ifuatavyo:

"(3) Mmiliki wa leseni au aliyesajiliwa atatunza kumbukumbu za wafanyakazi zifuatazo:

(a) kumbukumbu za ukasimishaji wowote wa majukumu; na

(b) kumbukumbu za mafunzo ya wafanyakazi katika kinga ya mionzi.".

Marekebisho ya kanuni 78

**8**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 78 kwa kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (4) kanuni ndogo mpya kama ifuatavyo:

"(5) Mmiliki wa leseni au aliyesajiliwa atahakikisha kwamba mwendeshaji wa kituo cha kuhifadhi au utupaji wa mabaki ya mionzi anaanzisha na kudumisha utaratibu unaotoa rasilimali fedha za kutosha kutekeleza majukumu yake.

(6) Mmiliki wa leseni au aliyesajiliwa atahakikisha kwamba-

(a) unafanyika ukaguzi wa mara kwa mara, usimamizi wa mabaki ya mionzi na matengezo ya kituo cha kuhifadhi mabaki hayo ili kuhakikisha ubora wake; na

(b) utoshelevu wa uwezo wa kuhifadhi mabaki ya mionzi unapitiwa mara kwa mara, kwa kuzingatia mabaki ya mionzi yanayotarajiwa kuzalishwa kutoka kwenye kazi za kawaida na matukio ya majanga kwa kutazama kipindi cha uhai wa kituo cha kuhifadhi mabaki ya mionzi na njia zilizopo za utupaji.".

Marekebisho ya kanuni 79

**9**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 79 kwa kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (6) kanuni ndogo mpya kama ifuatavyo:

"(7) Mmiliki wa leseni au aliyesajiliwa atahakikisha kwamba usalama unatathminiwa kwa vituo vyote

ambavyo usitishaji wa shughuli umepangwa kwa vituo vyote ambavyo vinaendelea na zoezi la usitishaji.

(8) Mmiliki wa leseni au aliyesajiliwa atachagua mkakati wa usitishaji ambao utakuwa msingi wa upangaji wa usitishaji ambao umezingatia sera na mkakati wa kitaifa wa usimamizi wa mabaki ya mionzi.".

Marekebisho ya kanuni ya 99

**10**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 99(4) kwa-

(a) kuongeza mara baada ya aya (b) aya mpya kama ifuatavyo:

"(c) anafanya uratibu baina ya mamlaka zenye majukumu yanayohusiana na kinga ya mionzi na usalama kwa hali zote za mmuliko wa mionzi; na"; na

(b) kubadili mpangilio wa aya (c) kuwa aya (d).

Marekebisho ya Jedwali la Tisa

**11**. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta na kuandika upya Jedwali la Tisa kama ifuatavyo:

"__________

JEDWALI LA TISA

_________

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 7(3)(d))*

Vizalisha mionzi vifuatavyo vinavyotoa mionzi isiyo ionishi vinasamehewa kutoka kwenye Kanuni hizi:

(a) Mionzi ya atraviolet (UV):

kifaa chochote kinachotoa mionzi ya sumakuumeme katika eneo la spektramu ya nanomita 180 hadi 400 kitasamehewa katika Kanuni hizi, ikizingatiwa kwamba uzito uliopimwa wa msongamano wa nguvu mawimbi uliotolewa (kama inavyopimwa katika umbali wa sentimita 5 kutoka sehemu yoyote inayofikika kwenye kifaa) haizidi 3 x $10^{-8}$ $W/cm^2$ *A, ambapo A ni kiwango cha uzani kilichotolewa katika Orodha ya 1 hapa chini:

Jedwali dogo la 1: Kiwango cha uzani A

| Urefu wa wimbi (nm) | A |
|---|---|
| 180 | 0.012 |
| 200 | 0.030 |
| 210 | 0.075 |
| 230 | 0.190 |
| 240 | 0.300 |
| 250 | 0.430 |
| 270 | 1.000 |
| 300 | 0.300 |
| 305 | 0.060 |
| 313 | 0.006 |
| 315 | 0.003 |
| 325 | 0.005 |
| 350 | 0.002 |
| 400 | 0.00003 |

Vidokezo vya kutumia Jedwali dogo la 1:

(i) Tumia njia ya kuweka msatari mnyoufu wa polinomia kwa urefuwimbi wa namba za kati.

(ii) Kwa vifaa vinavyotoa mionzi katika urefuwimbi zaidi ya mmoja, michango iliyopimwa kutoka kwa kila urefuwimbi inapaswa kujumlishwa.

(iii) Njia mbadala, vipimo vinaweza kufanywa na vifaa vyenye mwitikio wa sipektro ambao ulioundwa kulingana na viwango vya uzani vya Jedwali dogo la 1.

(b) Mionzi ya infraredi (IR):

Kifaa chochote kinachotoa mionzi katika masafa ya spektro nanomita 780 hadi milimita 1, chenye msongamano wa nguvu mawimbi wa chini ya 10 $mW/cm^2$, kama inavyopimwa kwa umbali wa sentimita 5 kutoka sehemu yoyote inayofikiwa kwenye kifaa.

(c) Mionzi ya masafa ya redio (RF):

| |
|---|
| Kifaa chochote kinachotoa mionzi ya masafa ya redio (RF) kati ya Kilohertz 100 na Gigahertz 300, ilimradi chanzo cha mionzi kina nguvu isiyozidi Wati 0.1, ikijumuisha: rimoti inayoendesha alamu ya gari kitasamehewa kutoka Kanuni hizi.”. |

Dodoma,
23rd December, 2024

ADOLF F. MKENDA,
*Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia*